HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI

# HAI YETU

**JARIDA TOLEO LA OKTOBA-DISEMBA 2022**









# WILAYA YA HAI YAKAMILISHA UJENZI WA MADARASA KWA WAKATI-MKUU WA MKOA AIPONGEZA



*Pichani ni kamati ya ulinzi na usalama ikiongozwa na mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro Nurdin Babu, mkuu wa wilaya ya Hai Juma Irando pamoja na viongozi wa idara mbalimbali wa wilaya ya Hai.*

Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro Nurdin Babu alipongeza wilaya ya Hai kwa kukamilisha ujenzi wa vyumba 10 vya madarasa ya sekondari ndani ya muda uliopangwa na kwa ubora huku akizitaka halmashauri zingine kujifunza kwa wilaya hiyo.

Akizungumza katika makabidhiano ya madarasa hayo yaliyofanyika katika Shule ya Sekondari Hai, Babu aliipongeza halmashauri hiyo kwakutumia kiasi cha fedha kilichotolewa na Serikali kwa kujenga madarasa yenye viwango sahihi yapatayo 10 na ofisi za waalimu katikati.

Pia Mkuu huyo wa Mkoa alitoa maagizo kwa halmashauri hiyo kuhakikisha kuwa mwezi Januari wanafunzi wote wanaotakiwa kuendelea na masomo wanafanya hivyo mara moja kwani Serikali imejenga madarasa hayo kwaajili ya wanafunzi hao na kinyume na hapo Serikali itachukua hatua kali kwa wale wote watakao kwamisha wanafunzi kujiunga na masomo mwakani.

Aidha aliagiza Halmashauri hiyo ya Hai na halmashauri zingine katika mkoa wa Kilimanjaro kutumia fedha za ndani za Halmashauri kukarabati madarasa chakavu huku akiwapongeza wananchi waliojitolea michangango yao mbalimbali ili kununua marumaru kwa ajilia kuongeza ubora wa majengo hayo.

Awali akimkaribisha Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mkuu wa wilaya ya Hai Juma Irando alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha za ujenzi wa madarasa katika wilaya ya Hai jambo ambalo limetatua tatizo la pungufu



*Jengo lenye vyumba vya madarasa manne shule ya sekondari Hai day*

wa madarasa na kwamba wanafunzi wote watakaochagulia kujiunga na elimu ya sekondari katika wilaya ya Hai hawatakosa nafasi.

Kwa upande wake mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Hai, Edmund Rutaraka alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuleta fedha nyingi za mradi katika wilaya ya Hai, hasa katika sekta ya Afya, barabara, Maji na elimu.

Naye mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilaya ya Hai Wang'uba Maganda alisema Serikali imeamua kuwekeza kwenye mambo ya maendeleo hasa huduma muhimu za kijamii na muda si mrefu changamoto nyingi za kijamii zitakuwa zimetatuliwa.

Awali akisoma taarifa ya ujenzi kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Hai Juma Irando, Mkuu wa divisheni ya Elimu Sekondari Julius Mduma alisema wilaya ya Hai ilipokea - milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 10 katika shule za Rundugai darasa moja , Hai madarasa matatu, Mukwasa darasa moja, Neema darasa moja, Tumo darasa moja, Longoi madarasa mawili, na Roo darasa moja.

Ujenzi wa madarasa yote umekamilka tayari kwa kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza Januari 2023.



*Muonekano wa ndani chumba cha darasa shule ya sekondari Hai day*

# TANI 420 ZA MAHINDI YA RUZUKU ZANUFAISHA KAYA 4478 WILAYANI HAI



*Mahindi ya ruzuku yakishushwa kwenye gari kwa ajili ya kuhifadhiwa na kuuzwa kwa wananchi wa wilaya ya Hai kwa bei nafuu*

Kaya 4,478 wilayani Hai zimenufaika na mahindi ya bei nafuu yaliyotolewa na Serikali kupitia wakala wa Taifa wa chakula NRFA kwa lengo la kusaidia wananchi kupunguza ukali wa maisha kufuatia kupanda kwa bei ya mahindi sokoni kutokana na kukosekana kwa mvua kwa misimu miwili mfululizo.

Afisa maafa wilaya ya Hai Msafiri Msuya alieleza kuwa hadi sasa wilaya hiyo imeshapokea tani 420 za mahindi na kuzigawa kwa wananchi kupitia viongozi wa vijiji na vitongoji kwa bei ya shilingi 44,000 kwa mfuko wa kilo 50.

"Niwaombe wananchi watumie fursa hii kwa ajili ya kujipatia hayo mahindi na wayatumie vizuri kwa matumizi ya nyumbani hapa tulipo hatujui kwamba msimu unaokuja, je tutalima? tutavuna? Kwa hiyo bado niwasihi, mahindi haya wayanunue na wayatunze"

"kwa upande wa viongozi hasa hawa wa vijiji nitumie fursa hii kuwaomba wawe waaminifu-kwamba mahindi haya yamekuja yanauzwa kwa bei nafuu ukilinganisha na bei ya sokoni, basi zile orodha ambazo wanaziandaa kule vijijini, wao ndio wako na jamii watusaidie kutuletea orodha sahihi ya wahitaji kweli kweli na wasifanye upendeleo"

"kama mtu hawezi kununua mfuko wa kilo 50 bado kule katika ngazi ya kitongoji wanaweza wakaungana familia kadhaa wakaorodheshwa wakajichanga na kila mtu akaweka kumbukumbu yake baadaye zikijumlishwa zinaweza zikafika mifuko miwili au mitatu wakagawana"

Akizungumza mwananchi wa kata ya Bomani Amosi Lema amesema wanamshkuru raisi Samia Suluhu Hasani kwa mahindi hayo ya ruzuku kwani asilimia kubwa ya wanachi hawakua na akiba ya chakula majumbani mwao.

Ikumbukwe kuwa mahindi hayo ya bei nafuu ambayo ni mkombozi wa wananchi hususani wa wilaya ya Hai huuzwa kwa 44,000 kwa mfuko wa kilo 50 na 88000 kwa mfuko wa kilo 100, huku bei ya sokoni huuzwa kwa shilingi 150,000.

# BABU AZINDUA ZOEZI LA UPIMAJI KIA



*Wataalamu wa upimaji wa maeneo wakiweka alama za mipaka katika eneo linalozunguka uwanja wa ndege wa KIA*

Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro Nurdin Babu amezindua rasmi zoezi la tathmini na upimaji kwenye eneo linalozunguka uwanja wa ndege wa kimataifa wa Kilimanjaro KIA lenye ukubwa wa kilomita za mraba 110 lililokuwa na mgogoro wa zaidi ya miaka 20 kati ya wananchi wanaozunguka uwanja huo na kampuni ya KADCO inayoendesha uwanja huo.

Zoezi hilo limelenga kumaliza mgogoro huo baada ya Serikali kusema kuwa baada ya tathmini hiyo itawalipa na kuwaondoa wananchi waliovamia eneo la uwanja huo.

Akiambatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya mkoa katika zoezi hilo lililoenda sambamba na uwekaji wa bikoni kutambua alama za mipaka Novemba 09, 2022, Mkuu wa Mkoa alieleza kuwa Serikali - inalenga kuendeleza uwanja wa KIA na ndiyo maana inafanya tathmini ya kuwabaini wale wote waliopo ndani ya uwanja huo walipwe fidia kupisha eneo hilo.

"Serikali inataka iendeleze uwanja wa KIA na ndiyo maana tunasema wale walioingia kwenye uwanja watatoka, lakini tutawajuaje? Lazima tufanye tathmini ili kubaini nani yuko ndani na nani yuko nje"

"Na nitoe wito, viongozi wa Serikali na wananchi wa KIA tutekeleze kwanza agizo la Serikali, tujue nani ameingia uwanjani na nani hajaingia baada ya hapo watakaobainika kuwa ndani ya uwanja hawataondoka hivi hivi, wote watafanyiwa tathmini watalipwa na wanalipwa kwa huruma pia ya Mhe. Rais kwa sababu uwanja huu una hati miaka 99"-



*Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro Nurdin Babu akizungumza na diwani wa kata ya Kia Tehera Molleli wakati wa uzinduzi wa zoezi la uwekaji wa alama za mipaka*

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi CCM Mkoa wa Kilimanjaro Patrick Boisafi aliwataka wananchi wa Kia kuwa wavumilivu na kutoa ushirikiano unaofaa wakati wa zoezi hilo ili kazi hiyo ifanyike kwa amani na utulivu.

Naye diwani wa kata ya Kia wilayani Hai Tehera Mollel aliiomba Serikali kuhakikisha kuwa wananchi wanaoondolewa katika eneo hilo wanatendewa haki "Mhe. Mkuu wa mkoa niendelee kukuomba kuwa, pamoja na kuwaondoa kwenye maeneo hayo wakazi wa Kia, tuwatendee haki"



*Wataalamu wa upimaji wa maeneo wakiwa wanapima eneo la KIA.*

# WEKENI TAARIFA ZENU WAZI KWA WANACHAMA – MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA HAI



*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Hai Dionis Myinga akizungumza kwenye mkutano wa ishirini na mbili (22) wa chama cha ushirika wa akiba na mikopo cha walimu wilaya ya Hai na Siha (H.T. SACCOS)*

Viongozi wa chama cha ushirika wa akiba na mikopo cha walimu wilaya ya Hai na Siha (H.T. SACCOS) wametakiwa kuwa wawazi na waadilifu katika uendeshaji wa chombo hicho kama katiba inavyoelekeza ili kuepuka migogoro baina yao na wanachama.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Hai Dionis Myinga ambaye alikuwa mgeni rasmi wakati wa mkutano wa ishirini na mbili (22) wa chama uliofanyika katika viwanja vya ofisi ya chama hicho.

"migogoro mingi huanzia kwenye fedha kwa kutokuwa waadilifu na wawazi katika uendeshaji wa shughuli za chama, katiba iheshimiwe, kutokusoma taarifa za mara kwa mara na ninyi wanachama lazima muwe wawazi katika uendeshaji wa shughuli zote na muwe waadilifu"Alisema Myinga

Myinga aliwataka wanachama wanaodaiwa wajitahidi kulipa madeni yao ili Saccos iweze kuendelea kujiendesha yenyewe na wanachama wanaodaiwa kujitahidi kulipa madeni hayo kwa wakati ili kuepuka kutetereka kwa chama hicho.

"wanachama mnaodaiwa mjitahidi kulipa madeni yenu ili saccos yetu iweze kusonga mbele , hapa mlipo mpo mbali nawapongezeni sana ila lazima tujitahidi kufanya vizuri zaidi tusibweteke tukarudi nyuma"Alisema Myinga

Kwa upande wake mwenyekiti wa Saccos Baraka Owenya aliwataka wanachama kujiwekea akiba mara kwa mara , kukopa kwa busara na kulipa kwa wakati , na kuwataka wanachama kuendelea kuhamasisha watu wengine kujiunga na chama hicho.



*Wanachama waliohudhuria mkutano wa ishirini na mbili (22) wa Chama cha ushirika wa akiba na mikopo cha walimu wilaya ya Hai na Siha (H.T. SACCOS)*

“bodi inawashukuru kwa dhati wanachama wote wanaoonesha uzalendo mkubwa kwa chama na kuhamasisha watu kujiunga na chama chetu , pili napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru watendaji wote wa chama kwa kujitahidi kusimamia chama chetu kwa uaminifu na kupelekea chama kuendelea kutengeneza faida”

“pia nawashukuru wadau mbalimbali, mkurugenzi mtendaji wa wilaya ya hai, na mrajisi wa vyama vya ushirika nchini , mrajisi msaidizi wa mkoa wa Kilimanjaro, maafisa ushirika hai na siha , maafisa elimu msingi na sekondari , chama cha walimu, shirikisho la vyama vya akiba na mikopo, saccos rafiki kwa ushirikiano wenu mkubwa katika kufanikisha shughuli za chama chetu”alisema Owenya

Naye mwenyekiti mstaafu wa chama hicho John Lengai aliwataka wanachama kushirikiana ,kushikamana na kuwaamini viongozi ili Saccos iweze kusonga mbele.

Mkutano huo wa ishirini na mbili(22) wa chama cha ushirika wa akiba na mikopo (saccos ) cha walimu wilaya ya Hai na Siha uliambatana na ugawaji wa vyeti kwa wanachama pamoja na upitishaji wa ajenda zote zilizojadiliwa.

Chama cha ushirika wa akiba na mikopo cha waalimu wa wilaya ya Hai na Siha kilisajiliwa mwaka 1993 na kuanza kufanya kazi mwaka 2001 kikiwa na wanachama 20 na mpaka kufikia mwaka huu wa 2022 kina wanachama 1407.

# MILA ZILIZOPITWA NA WAKATI KIKWAZO CHA KUKOMESHA UKATILI DHIDI YA WATOTO NA WANAWAKE



*Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Hai Edmund Rutaraka akizungumza kwenye kikao cha kamati ya Afya ya msingi kilichofanyika kwenye ukumbi wa halmashauri hiyo.*

Mila potofu, ushirikiano hafifu vimetajwa kuchangia vitendo vya ukatili hususani Kwa watoto kuendelea kushika kasi kwenye jamii na kurudisha nyuma juhudi za Serikali katika mapambano dhidi ya vitendo hivyo.

Akizungumza kwenye kikao cha Afya ya Msingi wilaya ya Hai kilichoketi kwenye ukumbi wa Halmashauri hiyo, mkuu wa wilaya ya Hai Juma Irando alionesha kushangazwa na baadhi ya jamii kuendelea kukumbatia mila zilizopitwa na wakati ikiwemo kutumia jani la sale kuomba msamaha na kumaliza vitendo vya ukatili vinapotokea, hali ambayo inamnyima haki mhanga wa tukio.

"Kwahiyo akishabeba tu hilo jani ni basi? hata kama ameua? Wananchi waendelee kuhamasishwa na kuelimishwa, wapewe elimu kwamba waachane na mila potofu, tuziepuke mila ambazo zinaonekana kuwa ni changamoto, twende na wakati"

Alitaka kesi zote ambazo upelelezi wake umekamilika zichukuliwe kwa uzito watuhumiwa wafikishwe mahakamani.

"tuachane na hii tabia ya kumaliza maliza kwa majani yenu haya (masale), fikisheni mahakamani, tukiona hatokei yule aliyeleta malalamiko, kapotea tu ghafla wakati tumefanya kazi kubwa ya kufanya uchunguzi achukuliwe hatua, haiwezekani unapeleka taarifa alafu -



*Afisa lishe wilaya ya Hai Happifania Laizer akichangia mada katika kikao cha kamati ya Afya ya msingi wilaya ya Hai.*

tunapeleka mahakamani unakuwa wa kwanza hutokei, kutoa taarifa ya uongo ni kosa kisheria"

Aidha mkuu huyo wa wilaya aliitaka jamii ikiwa ni pamoja na jamii ya kifugaji kuachana na mila na desturi potofu na za kizamani ikiwemo kuozesha watoto wadogo kwa nia ya kupata mahari kwani kufanya hivyo ni ukatili na unaokatisha malengo ya mtoto.

Kwa upande wake Katibu Tawala wilaya ya Hai Upendo Wella akizungumza kwenye kikao hicho, alitaka jamii kuchukua hatua madhubuti za kukataa na kukomesha vitendo vya ukatili hususani kwa watoto na watu wengine.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Hai Dionis Myinga alisisitiza kila mmoja kuendelea kuzuaia na kupambana na - vitendo vya ukatili kwa watoto na watu wote walioko kwenye hatari ya kufanyiwa vitendo hivyo.

Awali akiwasilisha taarifa ya ulinzi na usalama wa mtoto, Afisa ustawi wa jamii wilaya ya Hai Salome Zefania alitaja sababu za matukio ya ukatili kuongezeka, moja wapo ikiwa ni matumizi makubwa ya mila na desturi ikiwemo majani ya masale katika kusameheana vitendo vya ukatili na kuvimalizia nyumbani "hata aliyetoa taarifa ya ukatili, siku ya kutoa ushahidi hatokei mahakamani"

Naye mganga mkuu wa wilaya ya Hai Dkt. Itikija Msuya alisema wamejipanga kuendelea kutoa elimu ili kukabili vitendo vya ukatili kwani baadhi ya watu wanaofanya ukatili huo hasa kwa watoto, huwatishia -



***Kutoka kushoto ni mkuu wa wilaya ya Hai Juma Irando akifuatiwa na mwenyekiti wa Halmashauri hiyo Edmund Rutaraka na Mkurugenzi mtendaji wa halmashauri Dionis Myinga pamoja na mganga mkuu wa wilaya hiyo Dkt. Itikija Msuya kwenye kikao cha Afya ya msingi.***

kuwa watawaua na watoto wakitishiwa siyo rahisi kutoa siri kwa kuhofia maisha yao.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo Edmund Rutaraka akizungumza katika kikao hicho alisisitiza usimamizi thabiti ikiwa ni pamoja na uwazi wa fedha zinazotolewa na Serikali kwenye miundombinu ya afya na kuongeza kuwa wamepokea takribani bilioni 1.3 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya Afya.

Katika hatua nyingie Mkuu wa wilaya aliagiza jeshi la Polisi wilayani humo kufanya oparesheni kubaini mabanda ya video almaarufu vibanda umiza ambavyo vinatumika kuonesha picha zinazokwenda kinyume na maadili ili viweze kufungiwa lengo likiwa ni kunusuru kizazi cha sasa na baadaye

"Hivi vibanda vya video (vibanda umiza) OCD upo hapa, piteni chunguzeni na kufuatilia na kuona nini hasa kinafanyika huko, na vile ambavyo tunaona vinakwenda kinyume na maadili yetu tuvifungie”

"Kwanza sikuhizi si kila mtu ana TV yake nyumbani? Teknolojia imebadilika sikuhizi, ebu tuone Kama vinatusaidia, Kama havitusaidii tuvifungie, ebu fatilieni hili suala tuone ni namna gani tunaweza kubadilika kutoka kwenye mambo ya vibanda umiza na watu wawe na TV zao nyumbani ili ulinzi wa watoto uwepo"

# MMOMONYOKO WA MAADILI CHANZO CHA UKATILI KATIKA JAMII



*Diwani wa kata ya masama kusini Cedrick Pangani akiwa anazungumza kwenye kilele cha maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili.*

Ukosefu wa heshima, mmomonyoko wa maadili, mila na desturi kandamizi na kukosa hofu ya Mungu vimetajwa kuchochea vitendo vya ukatili katika jamii nyingi.

Akimwakilisha mkuu wa wilaya ya Hai kwenye kilele cha maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili, mkuu wa divisheni ya Mipango wilaya hiyo Said Abdallah alisema kuwa ni jukumu la kila mmoja kuchukua hatua kwa kupaza sauti kupinga vitendo vya ukatili ili kupunguza na hatimaye kutokomeza vitendo hivyo.

"Ni jukumu la kila mmoja kupaza sauti kupinga vitendo vya ukatili viavyotokea kwenye jamii hasa majumbani, kwenye taasisi mbalimbali, shuleni, kwenye usaafiri wa umma na sehemu ambazo si salama kwa wananchi"

"Matukio ya ukatili wa kijinsia bado yapo na yanatokea kwenye maeneo mbalimbali katika wilaya yetu ya Hai licha ya juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali katika kukomesha vitendo hivyo vinavyofanywa na watu wasiokuwa na mapenzi mema na wanawake na watoto"

"Natoa rai kwa kila mwananchi, sote tukatae ukatili wa aina yoyote pamoja kutoa ushirikiano pale uaktili unapotokea ili mhanga apate usaidizi mapema hususani matibabu na msaada wa kisheria.

Lakini pia msababishaji achukuliwe hatua za kisheria, kwani kufanya hivyo tutakuwa tumepunguza na kuondoa vitendo vya ukatili"



*Baadhi ya wananchi walioshiriki kwenye kilele cha maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili eneo la kwa Sadala.*

Kwa upande wake mkuu wa divisheni ya maendeleo ya jamii wilaya ya Hai Robert Mwanga akisoma risala kwa mgeni rasmi alieleza kuwa licha ya changamoto, halmashauri ya Hai kwa kushirikiana na wadau katika kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia wamefanikiwa kuwajengea wananchi na jamii uelewa wa kupunguza vitendo vya ukatili wa kijinsia.

"Elimu ya mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia katika ngazi ya vitongoji na kata imetolewa kwa njia ya mabango, vikao shuleni, na kwenye vyombo vya habari ikiwemo Redio Boma Hai fm"

Aidha alieleza kuwa katika kutoa Elimu ya kupinga ukatili, jumla ya watu 17,461 wamefikiwa kwa njia mbalimbali ikiwemo shule za msingi, shule za Sekondari, mikutano ya vijiji na Redio Boma Hai fm.

Maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili yakiongozwa na kauli mbiu isemayo "Kila Uhai una thamani, tokomeza mauaji na ukatili kwa Wanawake na Watoto" yamehitimishwa Disemba 10 katika eneo la Kwasadala na kuhudhuriwa na wananchi, taasisi za kupinga ukatili na viongozi mbalimbali akiwemo diwani wa kata ya Masama kusini Cedrick Pangani.

# SAASHISHA AOMBA WANANCHI KUTOA USHIRIKIANO KWA VIONGOZI



*Mbunge wa Jimbo la Hai Saashisha Mafuwe akiwa anazungumza na wazazi pamoja na walimu shule ya Lemira iliyopo kata ya Masama kati.*

Mbunge wa jimbo la Hai Saashisha Mafuwe amewataka wananchi wa wilaya hiyo kushirikiana na Serikali katika kuchangia shughuli za maendeleo ikiwa ni pamoja na shughuli za miradi ya Afya, Elimu na maji inayotekelezwa kwenye maeneo yao.

Saashisha aliyasema hayo kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika shule ya Sekondari Lemira iliyopo kata ya Masama kati na kueleza kuwa miradi hiyo inapokamilika huwanufaisha wananchi wote.

Aidha Mbunge huyo alitumia nafasi hiyo kuwataka viongozi wa vijiji vyote wilayani humo kuwasomea wananchi mapato na matumizi ili kuendelea kuwahamasisha wawe na mwamko wa kuchangia shughuli Za maendeleo.

“Niwaombe wazazi mlioko hapa tushirikiane na Serikali, tukiambiwa michango tutoe, na nyie mnisaidie kuhamasisha watu wachangie, kazi yangu ni kulinda visiliwe, kuhakikisha tunasomewa mapato na matumizi”

“Lakini mtu akisema eti mtu asichangie shughuli za maendeleo, huyo atufai wilaya ya Hai, muda wake wa kuishi wilaya ya Hai umeisha”

Naye diwani wa kata ya Masama kati Kandata Kimaro aliwaambia wananchi wa kata hiyo kuwa aliahidi kuwatumikia na hatoacha kuwatumikia wananchi hao huku akimuomba mbunge wa Hai Saashisha Mafuwe kuwasaidia ujenzi wa barabara ya lami Sadala-Lemira.

# WAKANDARASI WAAGIZWA KUKAMILISHA MIRADI KWA WAKATI



*Kamati ya ulinzi na usalama kutoka wilaya ya Hai ikiongozwa na mkuu wa wilaya Juma Irando katika ukaguzi wa miradi ya maendeleo.*

Serikali Wilayani Hai mkoani Kilimanjaro imewataka wakandarasi wa barabara kufanya kazi kwa weledi na kukamilisha ujenzi kwa wakati kwa mujibu wa mkataba baina yao na Serikali ili thamani ya fedha iweze kuonekana.

Mkuu wa Wilaya ya Hai ,Juma Irando alitoa Agizo wakati wa ziara yake ya kukagua miradi ya matengenezo ya barabara kwa mwaka fedha 2022/2023 inayosimamiwa na wakala wa barabara za Mijini na vijijini (TARURA) - ngazi ya wilaya hiyo.

Alisema wakandarasi wanawajibu mkubwa wa kutekeleza miradi kwa kiwango kinachostahili na kukamilisha kwa wakati ili jamii iweze kupata huduma stahiki na kuondokana na adha za miundo mbinu mibovu ya barabara.

Awali akitoa taarifa ya utekelezaji wa TARURA wilayani Hai,Kaimu Meneja Mhandisi Musa Sumbwe alisema kwa mwaka wa -

2022/2023 wanatekeleza mikataba sita ya matengenezo ya barabara yenye thamani ya zaidi ya Shilingi bilioni 4.8.

Sumbwe alisema kati ya miradi hiyo upo mradi wa matengenezo wa barabara kwa kiwango cha lami ya Makoa Darajani- TaCRI-Mferejini unaotarajiwa kutumia zaidi ya bil 2.9 ambao unatekelezwa na Serikali kupitia fedha za maendeleo za tozo ya mafuta.

Alifafanua kuwa kwa sasa kazi inayoendelea ni kupasua miamba ambapo ujenzi wa barabara hiyo unatekelezwa na mkandarasi Builders and Limeworks Ltd unaotarajiwa kukamilika April 25 mwaka 2024.



*Miongoni mwa madaraja yanayojengwa kwenye barabara za wilaya ya Hai ikiwa ni sehemu ya kuborseha huduma ya usafirishaji.*

# WATUMISHI WA AFYA WATAKIWA KUIMARISHA HUDUMA



*Mbunge wa jimbo la Hai Saashisha Mafuwe aliyevaa kofia nyeusi akiwa anasalimiana na wagonjwa Hospitali ya wilaya ya Hai wakati wa ziara yake ya kikazi.*

Mbunge wa Jimbo la Hai Saashisha Mafuwe amewataka watumishi wa Hospital ya wilaya ya Hai kutoa huduma nzuri kwa wagonjwa na kutumia lugha nzuri.

Saashisha aliyasema hayo Disemba hiyo 15 2022 na kusema kuwa lengo la kufika katika Hospital hiyo kuona Maendeleo ya fedha za Serikali pamoja na kuzungumza na watumishi Hao.

Saashisha alisema kuwa watumishi hao waliahaidi kufanya kazi kwa weledi na kuimarisha huduma za afya pamoja na kuwa na lugha nzuri kwa wagonjwa, na kuwa dawa zipo kwa asilimia 97.

"Tumepata muda wa kuzungumza vizuri na watumishi wote wa hospitali hii na wamehaidi kutoa huduma nzuri pamoja na kutumia lugha nzuri kwa wagonjwa wetu, hivyo ni Imani yangu kwamba wananchi wanaenda kupata huduma inayostahili, hivyo niwatoe hofu wananchi wa Jimbo la Hai kwani watumishi wamehaidi wenyewe na watakwenda kuimarisha huduma."

Pia alimshukuru Mhe Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa fedha alizoleta katika jimbo la Hai kwenye sekta ya afya kiasi cha shilingi Bilioni 1.3 na hospital ya Wilaya imepata shilingi milioni 900 kwa ajili ya matengenezo na majengo matatu pamoja na njia za kuunganisha jengo kwa jengo, kujenga kichomea taka ambacho

kilikua kero kwa wananchi.

Kwa Upande wake Diwani wa Kata ya Bomang'ombe Evod Njau alisema kuwa wamepokea shilingi milioni 900 kwa ajili ya hospital ya Wilaya ya Hai na kuwa fedha iyo itatumika kama ilivyokusudiwa.

Nae Mganga Mfawidhi wa Wilaya Ya Hai Dkt. Grace Charles amesema kuwa wamepokea yale yote mbunge aliyoagiza pamoja na kuwasimamia watumishi ili waweze kutoa huduma nzuri na kuwa na lugha nzuri kwa wagonjwa.
Pamoja na Mhe. Mbunge kufanya ziara katika hospitali hiyo pia ametembelea wagonjwa katika wodi na wagonjwa wa nje.



***Baadhi ya madaktari wa Hospitali ya wilaya ya Hai wakiwa kwenye mazungumzo na Mbunge wa jimbo la Hai Saashisha Mafuwe.***

# UTALII CHANZO CHA MAPATO



*Viongozi wa Divisheni mbalimbali kutoka halmashauri ya wilaya ya Hai wakiwa wanavuka daraja la mungu.*

Utalii wa ndani umekua ukihimizwa na viongozi mbalimbali ikiwemo wa Halmashauri ya wilaya ya Hai ikiwa njia nzuri ya kuongezea Taifa pato pamoja na kuthamini rasilimali za taifa.

Hayo yamebainika baada ya timu ya wataalam halmashauri ya wilaya ya Hai kutembelea eneo linaloitwa Sieni lilipo Masama katika ziara iliyolenga kutembelea vivutio mbali mbali vya utalii kwa lengo la kuangalia namna ya kuviboresha na hatimaye kuanza kutumika.

Akizungumza katika ziara hiyo Afisa utalii wilaya ya Hai Amani Temu alisema vivutio hivyo vya utalii - ni muhimu kwa wilaya ya Hai endapo vitaboreshwa kutokana na historia ya eneo hilo kuwa ni ya kipekee kwani kuna eneo ambalo linaitwa daraja la mungu ambalo ni daraja lililojijenga lenyewe kwa mawe pekee.

“watalii watatamani kuja hapa kuona hilo daraja la mungu lipoje na kwanini liitwe hivyo kuna historia gani hapa hiyo ni hatua tosha ya kuongeza pato la nchi kwa watalii wa ndani na wa nje wakija hapa kuona daraja hili, kwakweli tuthamini vya kwetu”.

Miongoni mwa watu waliokuwa kwenye ziara hiyo ni mchungaji Walter Kimaro aliyeishi katika eneo hilo kwa muda mrefu na kuelezea kuwa eneo hilo ni sehemu ambayo watu walikuwa -



***Daraja La Mjerumani***

wanaenda kufanya ibada na kuomba baadhi ya vitu huku wakienda wakati mwingine wanavikuta.

Ameongeza kuwa eneo hilo lilikuwa na mapango ambayo watu walikua wanajificha wakati wa vita vya wenye kwa wenyewe(wamachame na wakibosho).

Pia eneo hilo lilikuwa likitumika kuangalia utabiri wa matukio ya mwaka kama vile njaa, ugonjwa, ukame pamoja na mvua lakini kwa zama za sasahivi hicho kitu hakipo tena.

“nilifahamu eneo hili mwaka wa 61 nikiwa mdogo sana kipindi hicho ukitaka kuongea na mababu lazima uingie huko kwenye mapango , walikuwa wanaenda na vitu vya kuchinjachinja na pombe saa nyingine , na sio kila mtu alikua anapaswa kuingia huko ilikua ni watu maalumu na mpaka ukristo ulipoingia waliacha mila hizo zilionekana hazina maana japo kweli ulikua ukiomba unapata kabisa”.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa wilaya ya Hai David Lekei alisema anatambua eneo hilo kama eneo muhimu sana na maeneo kama hayo ni lulu kwa taifa na ni maeneo ya kipekee ya kuweza kutuingizia kipato.

“ tunashukuru sana kwa mapokezi tuliyopata nadhani hili eneo linapaswa liandikiwe historia ili watalii wakianza kuja wapate historia kamili hili eneo ni la kipekee kwakweli siajawahi kuona eneo kama hili nashukuru sana uongozi wa kijiji pamoja na uongozi wa halmashauri ya wilaya ya Hai kwa kuweza kushirikiana kufahamu sehemu kama hii hivyo tuhimizane tuanze wenyewe kuwa watalii na tuyatunze haya maeneo kwa vizazi vijavyo na kwa Taifa pia kwenye kuongezea pato nchi hili eneo liandikiwe historia kwakweli naomba sana”.

# BARABARA YA NYERERE KUJENGWA



*Kamati ya ulinzi na usalama kutoka wilaya ya Hai ikiongozwa na Mkuu wa wilaya Juma Irando katika ukaguzi wa miradi ya maendeleo na hapa ni barabara ya nyerere.*

Mwenyekiti wa halmashauri ya wilaya ya Hai Edmund Rutaraka amesema kuwa wilaya hiyo imeweka mikakati madhubuti ya kusogeza maendeleo kwa wananchi ambapo tayari wamempata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya nyerere Bomang'ombe yenye urefu wa mita 700.

Rutaraka ambaye ni diwani wa kata ya Muungano, alieleza hayo wakati akizunguza kwenye kikao na kamati ya siasa ya CCM kata ya Muungano kilichoketi kwa lengo la kujadili mapendekezo ya kuanzishwa kwa - ujenzi wa ofisi ya CCM kata hiyo kilichofanyika shule ya msingi Mlimashabaha na kuongeza kuwa barabara hizo zinazowekewa lami zitawekwa taa za barabarabani.

"Tunaendelea kufanya kazi, Dorcas barabara inaongezwa kipande cha lami mita 200 ambacho kitafika hadi kwenye ile njia ya kwenda kwa Palanjo na mwakani tutaanza mazungumzo kwa ajili ya kuweka lami barabara ya Ngalawa kipande kilichobaki kutoka kwa mkuu wa wilaya, hospitali hadi kutokezea barabara ya Sanya Juu mita 400 tumeweka



*Kamati ya ulinzi na usalama ikikagua barabara ya nyerere ambayo ipo wilaya ya Hai.*

pale fedha, kuna milioni 300 tunamalizia barabara ili iunganike ya lami" amesema Rutaraka."Wale wanaofanya biashara barabara ya Nyerere ile barabara tayari mkandarasi ameshapatikana tunaweka lami pale mita 700 kuanzia stendi ya Bomang'ombe hadi kutokezea barabara ya Arusha, lakini pia tumepanga kuweka lami mita 200 kutoka stendi ya Rundugai kuelekea weekend"

"Vilevile milioni 300 tayari zimetengwa kwa ajili ya kuweka lami barabara ya Snow view-Rundugai mita 500 na barabara ya Rundugai-TPC imeshaombewa fedha kwa ajili ya kuweka lami kilomita 26 na barabara zote hizi zinazowekwa lami zitawekewa taa, kwa hiyo usiku hakutakuwa tena na giza kwenye barabara" ameongeza Rutaraka.

Kwa upande wake Katibu wa Itikadi, Siasa na Uenezi wa CCM wilaya ya Hai Muddy Msalu akielezea utekelezaji wa Ilani ya chama hicho, ameeleza kuwa Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan imeweka mipango madhubuti kwa ajili ya kuwaletea wananchi wa wilaya hiyo maendeleo.

# HALMASHAURI YATOA POLE KWA WATUMISHI WALIOUNGULIWA NYUMBA



*Miongoni mwa nyumba za walimu zilizoungua na moto usiku wa kuamkia disemba 29.*

Halmashauri ya wilaya ya Hai imekabidhi kiasi cha shilingi milioni mbili kwa familia mbili za walimu kufuatia ajali ya moto uliozuka majira ya saa 8 usiku wa kuamkia Disemba 29, 2022 na kuchoma nyumba waliyokuwa wakiishi pamoja na vitu vyote vilivyokuwamo ndani ya nyumba hiyo katika kitongoji cha Nyerere kata ya Muungano wilayani humo.

Akikabidhi fedha hizo kwa waathirika wa ajali hiyo ya moto, Mwenyekiti wa halmashauri ya wilaya ya Hai Edmund Rutaraka ambaye pia ni diwani wa kata ya Muungano alitoa pole kwa familia hizo na kuwataka kuwa na subira ikiwa ni pamoja na kumshukuru Mungu kwa kuwa hakuna vifo wala majeruhi.

“Sisi kama halmashauri ya wilaya ya Hai tumeona tuje tuwashike mkono kwa - kiasi cha shilingi milioni moja kwa kila familia ili muweze kuona ni kitu gani cha muhimu cha kuanza kufanyia kazi haraka wakati tunaendelea kuwatafuta wadau mbalimbali kuweza kusaidia familia hizi, poleni sana na tunaamini ni mipango ya MwenyeziMungu kwa sababu pameungua lakini hakuna kifo wala majeruhi yoyote”

Mkurugenzi mtendaji wa halmashauri hiyo Dionis Myinga akizungumza katika eneo la tukio asubuhi aliwapa pole kwa kupotelewa na mali zao zote kufuatia ajali hiyo ya moto na kueleza kuwa.

“baada ya kuwa wamepotelewa mali zao zote kwa ajali hii ya moto kimsingi bado wanahitaji mahitaji mbalimbali kama vile chakula, malazi na mavazi hivyo kama halmashauri tukaona ni busara tuangalie chochote kinachoweza kupatikana kwa ajili yao”

Akizungumza baada ya kukabidhiwa fedha hizo, Rahel Shedafa kwaniaba ya familia hizo alishukuru viongozi wa Halmashauri Kwa kuwambilia katika kipindi kigumu wanachopitia.

Walimu hao Zanika Solomon na Raheli Shedafa walikuwa wamepanga katika nyumba inayomilikiwa na wakala wa majengo Tanzania TBA ambapo nyumba hiyo pamoja vitu vyote vilivyokuwa ndani vimeteketea kwa moto ambao ulizuka usiku wa manane na chanzo chake bado hakijajulikana.





*Familia zilizokutwa na maafa ya moto zikipokea fedha kutoka kwa viongozi wa Halmashauri ambapo aliyevaa miwani ni mwenyekiti wa halmashauri Edmund Rutaraka na kutoka kulia ni mkurugenzi wa Halmashauri ya Hai (W) Dionis Myinga.*

# WANAUME HAI WATAKIWA KUPIMA AFYA NA WAKE ZAO



*Viongozi kutoka Halmashauri wakiwa katika kilele cha maadhimisho ya siku ya ukimwi duniani*

Afisa tawala wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro Mary Mnyawi amewasihi wanaume kujitokeza kupima afya Kwa pamoja na wake zao huku akiwataka kuacha kutegemea majibu ya wake zao pale wanapokwenda kupima afya hasa wakati wa ujauzito.

Mnyawi aliyasema hayo kwenye kilele cha maadhimisho ya siku ya Ukimwi duniani ambayo huadhimishwa duniani kote Disemba 01 ya kila mwaka ambapo katika wilaya ya Hai maadhimisho hayo yalifanyika katika viwanja vya Snow view Bomang'ombe.

"Wanaume msitegemee kwamba majibu ya wake zenu wanapokwenda kupima ndiyo majibu ambayo yanatosha kukuonyesha wewe upo salama, na kama yeye je anao? Lakini inawezekana mmoja akapata na mwingine asipate inategemea na kinga ya mtu ilivyo" amesema Afisa tawala Mnyawi

"kwahiyo ninawasihi sana muwe na tabia ya kwenda kupima kwa pamoja ili kuona na kujua afya zetu zikoje ili baada ya hapo pia tuweze kuelimishwa na kujua namna gani ya kuenenda nab ado tunakuwa na muda mrefu tu wa kuishi hapa duniani vinginevyo ni rahisi kudondoka kwa ghafla kwa kuwa hujafanya kile ambacho ungeelekezwa na wataalamu wa afya"



*Baadhi yawananchi waliohudhuria kwenye kilele cha maadhimisho ya siku ya ukimwi duniani*

Akizungumzia mapambano dhidi ya Ukimwi, Mnyawi alieleza kuwa wilaya hiyo imefanikiwa kuwaanzishia dawa za kufubaza makali ya virusi hivyo ARV's asilimia 94% ya waathirika kati ya 95% ya waathirika waliogundulika kuambukizwa.

Siku ya Ukimwi jumla ya watu 736 walipimwa katika wilaya ya Hai, wanaume wakiwa 242 na wanawake 494 ambapo waliogundulika kuwa na maambukizi ni ya VVU ni 15, wanaume 6 na wanawake 9 hali ambayo inaonyesha kushuka kwa maambukizi kwani waliopima ni wengi ila waliogundulika kuambukizwa ni wachache.

Akizungumza katika maadhimisho hayo, makamo wa mwenyekiti Halmashauri ya wilaya ya Hai Swalehe Kombo Sway ambaye pia ni mwenyekiti wa kamati ya kudhibiti Ukimwi wilayani humo anasema kwamba

"tumekaa, tumejaribu kupanua wigo mpana wa kuhakikisha kwamba jamii nzima ya wilaya ya Hai inapata elimu ya kutosha juu ya ugonjwa huo"

Mratibu wa ukimwi hospitali ya Hai Dkt. Macha wakati akitoa taarifa ya hali ya ugonjwa huo ameeleza kuwa kuna mwitikio hasi kwa wanaume kwamba majibu ya wenza wao ndiyo majibu yao, hali ambayo imekuwa ikidhoofisha jitihada za Serikali katika kufikia malengo ya kutokuwa na maambukizi mapya ifikapo mwaka 2030.

Mganga mkuu wa wilaya ya Hai Dkt. Itikija Msuya amewataka wale wote ambao tayari wameambukizwa virusi vya ugonjwa huo kufuata kwa usahihi maelekezo na kanuni za kitabibu ili maisha yaendelee kama kawaida kwani wapo watu wengi ambao wameambukizwa lakini wanafuata maelekezo ya wataalamu wa afya na wanaendelea kuishi.

# WANANCHI NA VIONGOZI WA VIJIJI WASISITIZWA UTUNZAJI WA MITI, HAI



*Katibu tawala wilaya ya Hai Upendo Wella akiwa anapanda mti katika wiki ya maadhimisho ya miaka 61 ya uhuru wa Tanganyika .*

Serikali wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, iliagiza viongozi wa vijiji pamoja na wananchi kuhakikisha kuwa wanatunza miti inayooteshwa ili kuboresha mazingira pamoja na kukabiliana na ukame katika maeneo mbalimbali.

Agizo hilo lilitolewa kwa nyakati tofauti na Katibu tawala wa wilaya ya Hai,Upendo Wella kwa niaba ya mkuu wa Wilaya Juma Irando, katika zoezi la upandaji miti kwenye wiki ya maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru wa Tanganyika .

Alisema zoezi la kupanda miti limekuwa - likifanywa kila mara na jamii imekuwa ikipanda kwa ajili ya maadhimisho na kusahau jukumu la kuitunza jambo ambalo limesababisha kuendelea kuwa na mazingira ya ukame.

Alisema kutokana na wananchi kupanda miti pasipo kuitunza kunafanya nchi kuendelea kuwa jangwa pamoja na kusababisha vyanzo vya maji kukauka na mazingira ya maeneo ya makazi kutokuwa bora.

“Miti iliyooteshwa inatunzwa na haikatwi hovyo, na hatua kali zitachukuliwa kwa yeyote atakaye kata miti hovyo pasipo



***Katibu tawala wilaya ya Hai Upendo Wella akiwa anapanda mti katika wiki ya maadhimisho ya miaka 61 ya uhuru wa Tanganyika***

kuzingatia kanuni na taratibu zilizowekwa na Serikali"alisema Upendo wella

Kwa upande wake Afisa Maliasili Wilaya ya Hai, Mbayani Mollel aliwakumbusha viongozi wa vijiji kutunza na kuilinda miti iliyooteshwa ambayo itasaidia kutunza mazingira kwa faida ya kizazi cha sasa na cha baadaye huku akiahidi kuwapa ushirikiano pale watakapohitaji msaada wa kitaalamu katika utunzaji wa mazingira.

Maadhimisho ya miaka 61 wilaya Hai yalifanyika kwa kufanya shughuli mbalimbali ikiwemo kufanya usafi ,kuotesha miti 300 kwenye Vituo vya Afya vya Chekimaji na Longoi.

# MATUKIO KATIKA PICHA



*Kamati ya ulinzi na usalama ikiongozwa na mkuu wa wilaya ya Hai Juma Irando kukagua miradi ya maendeleo*



*Wajumbe wa kamati ya Fedha,Uongozi na mipango wakikagua mradi wa maendeleo soko la Gezaulole.*

# MATUKIO KATIKA PICHA



*Jengo lenye vyumba vya madarasa manne shule ya sekondari Hai day*



*Muonekano wa ndani chumba cha darasa shule ya sekondari Hai day*

# MATUKIO KWA PICHA




Mbunge wa Jimbo la Hai Mhe. Saashisha Mafuwe akikagua barabara ya Bomang'ombe, Chekimaji-TPC



Wajumbe wa kamati ya Fedha wakikagua tenki la maji la mradi wa uboreshaji na upatikanaji wa maji Hai Mjini

# MATUKIO KATIKA PICHA



Jengo la kuhudumia wagonjwa wanaohitji uangalizi maalum(ICU)



Jengo la kuhudumia wagonjwa wanaohitji uangalizi maalum(ICU)

# MATUKIO KATIKA PICHA



Halmashauri ya Wilaya ya Hai ilipokea gari jipya kwa ajili ya kurahisisha ufuatiliaji wa shuguli za mpango wa kunusuru kaya masikini (TASAF)



Ukarabati na umaliziaji wa shule ya ufundi chekimaji vyumba viwili vya madarasa na ofisi moja kutokana na TASAF

# MATUKIO KATIKA PICHA



Ukarabati na umaliziaji wa choo shule ya ufundi Chekimaji kupitia fedha za mpango wa kunusuru kaya masi-kini (TASAF) kazi inaendelea



Ukarabati na umaliziai wa choo shule ya ufundi cheki maji kupitia mpango wa kunusu kaya masikini (TASAF) kazi inaendelea

HALMASHAURI YA WILAYA
HAI
DISTRICT COUNCIL

KAZI

**JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI.**

**S.L.P 27, Hai ,Kilimanjaro, Tanzania**

www.haidc.go.tz Hai Dc

http://radiotadio.co.tz/bomahaifm

Radio Boma Hai Fm 89.3 Mhz